



Na Mwandishi Wetu

Muongwana Lazima Nilonge

Tupatiwe daladala Goba, Makongo

TUNALONGA na kuwasalimu maofisa wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Ardhi (LATRA), meya wa halmashauri za Kinondoni na Ubungo pamoja na Wizara ya Ujenzi, tukiwasilisha maombi ya kuomba huduma ya mabasi ya daladala, kwa sababu kwa muda mrefu kimekuwa ni kilio kwetu.

Ni sisi wakazi wa eneo lililo kati Makongo Juu na Goba, Dar es Salaam, ambao licha ya kumalizika kwa barabara kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi kupitia Makongo juu Hadi Goba Senta, hakuna usafiri wa daladala na hali hiyo inadumu kwa muda mrefu karibu miaka 10 sasa.

Wakazi wa maeneo kuanzia Makongo Juu hadi Goba Senta tunaumia kwa kukosa usafiri wa daladala na kulazimika kutumia bajaji au bodaboda kwa wenye kipato, lakini walio na uchumi usioruhusu wanatembea umbali mrefu.

Viongozi wafikirieni wazee, wagonjwa, wajawazito na wazazi, wanafunzi na wanaopatwa na dharura nyingine ni nini hatima yao katika mazingira hayo? Hakika hali si shwari na wengi wameumia kutokana na kusahaulika.

Tunalalamika kwa sababu mambo yamekuwa magumu nyakati hizi ambazo gharama za mafuta zimepanda na kusababisha kila dereva wa bajaji au pikipiki kupanga bei anayoitaka.

Tunaikumbusha Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Ardhi kuwa licha ya kwamba tupo Dar es Salaam tena kwenye barabara zenye lami tunaendelea kukumbwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa huduma ya uhakika ya usafiri wa mabasi ya umma. Tunaomba itangaze ruti ili daladala zianze kutuhudumia.

Licha ya maeneo haya kukua kwa kasi kwa idadi ya watu pamoja na shughuli za kiuchumi kama shule, hoteli, vituo vya mafuta, masoko na maduka bado miundombinu ya usafiri haijaendana na mahitaji halisi ya wakazi wake ambao

wangetamani kuwe na mabasi kutoka Makumbusho hadi Goba mpaka Mbezi kupitia barabara ya Chuo Kikuu cha Ardhi hadi Makongo Juu kisha Goba hadi Mbezi Magufuli.

Ni jambo linalotuchosha kuona wananchi tunateseka kila siku tukisubiri usafiri kwa muda mrefu, kulazimika kupanda vyombo visivyo rasmi, au kutumia gharama kubwa kufika katikati ya jiji na maeneo mengine ya kikazi. Hali hii si tu inapoteza muda wa uzalishaji bali pia inaongeza gharama za maisha kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati.

Kutokana na hali hiyo, tunaomba Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhi (LATRA) kuchukua hatua za haraka kuhakikisha huduma za mabasi zinapatikana kwa uhakika katika maeneo ya Goba na Makongo. Hatua hii inaweza kujumuisha kuongeza idadi ya mabasi yanayofika maeneo hayo, kuboresha ratiba za safari, pamoja na kuruhusu waendeshaji zaidi kutoa huduma katika njia husika.

Aidha, uwapo wa mabasi ya uhakika utasaidia kupunguza msongamano wa magari barabarani, kuboresha usalama wa abiria, na kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa wakazi wa maeneo hayo. Ni muhimu kutambua kuwa usafiri wa uhakika ni mhimili muhimu katika maendeleo ya miji na ustawi wa wananchi wake.

Tunaomba LATRA na Wizara ya Ujenzi kusikiliza kilio cha wakazi wa Goba na Makongo na kuchukua hatua stahiki kwa manufaa ya jamii na maendeleo ya jiji la Dar es Salaam kwa ujumla, tunajuiliza mbona wenzetu wanaoishi kati ya External, Makuburi, Maji Chumvi hadi Korogwe wana mabasi tena yakianza safari Mbezi hadi Kariakoo kupitia Kigogo hadi Msimbazi inakuwaje sisi tunasahaulika?

Ni kwa niaba ya Wananchi waishio kati ya Goba Senta na Makongo Juu Dar es Salaam.

Tunalalamika kwa sababu mambo yamekuwa magumu nyakati hizi ambazo gharama za mafuta zimepanda na kusababisha kila dereva wa bajaji au pikipiki kupanga bei anayoitaka.